# الذَّكَاةُ وَشُرُوْطُهَا

# KUCHINJA NA MASHARTI YAKE

**Mwandishi:**

**Abu Halima Arafaat**

**(Allaah amsamehe yeye na wazazi wake)**

**0715263253.**

## UTANGULIZI WA MWANDISHI

Kila sifa njema anastahiki Allaah bwana wa viumbe wote, na swala na salamu zimshukie Nabii wa umma huu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba pia.

**Baada ya hayo:** tumetanguli kutaja hukumu mbalimbali kuhusiana na mnyama anayefaa kuchinjwa katika Udh-hiya, katika Makala yetu iliyopita (Makala namba 1), na nataraji kuwa ndugu zangu wamenufaika na kile ambacho tumekitaja ndani ya Makala hiyo.

Kama inavyofahamika kwamba kuchinja mnyama kwa ajili ya Udh-hiya ni ibada kubwa iliyo himizwa na sharia yetu tukufu, na haikubaliwi ibada yoyote isipokuwa kwa kukamilisha masharti yaliyowekwa kisheria, kinyume ya hivyo utakuwa umefanya upuuzi na hakuna malipo yoyote mbele ya Allaah 'Azza Wajalla.

Kwa ajili hiyo kwa taufiq ya Allaah nimeona kwa kukamilisha maudhui hii nilezee pia suala la kuchinja na masharti yake, kwa sababu huenda mtu akamiliki mnyama ambaye anatosheleza katika Udh-hiya lakini akawa hajui masharti ya kuchinja na adabu zake pia, ikawa ni sababu kwake kufahamu au kudiriki lile alilosahau.

Namuomba Allaah ajaalie aweke katika amali yangu hii Ikhlaas na kupatia mwenendo wa Mtume swala na salamu zimshukie kwenye kile ninachokusudia kuandika, hakika yeye Allaah ni Muweza juu ya hilo.

Wabillaahi Ttaufiiq.

بسم الله الرحمن الرحيم

**Kuchinja ni:** kumwaga damu ya mnyama wa Nchi kavu aliye halali, kwa kumchinja, (au kufanya) nahru au kumjeruhi sehemu yoyote ya mwili wake.

**Nahru:** inakuwa kwa ngamia, kwa kumtoboa chini ya shingo yake.

**Ama kujeruhi:** ni kwa mnyama yoyote ambaye haiwezekani kuchinjwa kwa njia ya kawaida, sawa awe ni ngamia, ng'ombe n.k.

Kwa mnyama wa aina hii tuliyotaja ili awe ni halali kuliwa lazima yapatikane masharti yafuatayo kwa mchinjaji:

1. Awe mchinjaji ni miongoni mwa wenye uwezo wa kukusudia kuchinja, kama vile kuweza kupambanua (kujua linalofaa na lisilofaa), kuwa na akili timamu, n.k, kwa hiyo haitofaa kuchinja mtoto mdogo au mtu mzima sana ambaye hawezi kupambanua, kadhalika mwenda wazimu na mlevi.
2. Awe mchinjaji ni muislamu au Ahlul kitaab (mtu anayejina dini ya Uyahudi au Unaswara)[1], ama muislamu itajuzu hata kama ni faasiki (muovu), mtu anayefanya bidaa ambayo haimtoi katika uislamu, aua mtoto mdogo mwenye kupambanua, au mwanamke.

Amesema Ibnul Mundir Allaah amrehemu:

«وَأَجْمَعُواْ عَلَى إِبَاحَةِ ذَبِيحَةِ الصَّبِيِّ وَالْمَرْأَةِ إِذَا أَطَاقَا الذَّبْحَ، وَأَتَيَا عَلَى مَا يَجِبُ أَنْ يُؤْتَى عَلَيْهِ»

[1]- Endapo watalitaja jina la Allaah juu yake.

**"Wamekubaliana juu ya uhalali wa mnyama aliyechinjwa na mtoto mdogo au mwanamke ikiwa wataweza kuchinja, na kufanya yale yaliyo wajibu kuyafanya (wakati wa kuchinja)[2]".**

Ndiyo maana Ibn Qudama Allaah amrehemu aliponukuu maneno haya katika kitabu chake pamoja na kutaja hadithi ya mjakazi wa Kaab Ibn Malik Allaah amridhie aliyechinja mbuzi kwa jiwe na Mtume swala na salamu akalikubali jambo hilo, akasema:

**«وَفِي هَذَا الْحَدِيثِ فَوَائِدُ سَبْعٌ: أَحَدُهَا، إبَاحَةُ ذَبِيحَةِ الْمَرْأَةِ»**

**"Katika hadithi hii kuna faida saba: ya kwanza ni: uhali wa kichinjwa cha mwanamke[3]".**

Amesema Ibn Hazmi Allaah amrehemu:

**«وَلَا أَعْلَمُ خِلَافًا فِيْ أَكْلِ مَا ذَبَحَتِ الْمَرْأَةُ الْمُسْلِمَةُ الْعَاقِلَةُ الْبَالِغَةُ عَلَى الشُّرُوْطِ الَّتِيْ ذَكَرْنَا فِيْ الرَّجُلِ»**

**"Wala sijui khilafu yoyote kuhusu (kufaa) kula mnyama aliyechinjwa na mwanamke, muislamu, mwenye akili, baleghe, juu ya masharti ambayo tumeyataja kwa mwanamme[4]".**

Amesema Imam Nnawawi Allaah amrehemu:

**«وَيَجُوزُ أَنْ يُوَكِّلَ كِتَابِيًّا وَامْرَأَةً وَصَبِيًّا .... وَفِي كَرَاهَةِ تَوْكِيلِ الْمَرْأَةِ الْحَائِضِ وَجْهَانِ (أَصَحُّهُمَا لَا يُكْرَهُ لِأَنَّهُ لَمْ يَصِحَّ فِيهِ نَهْيٌ»**

[2]- Al-ijmaa (Uk. 75).
[3]- Al-Mughni (Jz. 9, Uk. 402).
[4]- Maraatibul ijmaa (Uk. 147).

**"Na inajuzu kumuweka uwakala (katika kuchinja) Ahlul kitaab (Myahudi au Mnaswara), mwanamke na mtoto mdogo, …… na kuhusu uwakala kwa mwanamke mwenye hedhi kuna kauli mbili na iliyo sahihi zaidi si karaha, kwa sababu hakuna kuhusiana na hilo katazo lolote (kisheria)[5]".**

Bali huo ndio msimamo wa Jumhuri (maulamaa walio wengi) kama alivyosema Imam Shaukani Allaah amrehemu akifafanua maneno ya Mtume swala na salamu zimshukie alipoamrisha Kaab Allaah amridhie kula myama huyo aliyechinjwa na Mjakazi:

**«فِيهِ دَلِيلٌ عَلَى أَنَّهَا تَحِلُّ ذَبِيحَةُ الْمَرْأَةِ، وَإِلَيْهِ ذَهَبَ الْجُمْهُورُ»**

**"Katika hadithi hii kuna ushahidi juu ya uhalali wa kichinjwa cha mwanamke, na huo ndiyo msiamo wa Jumhuri (maulamaa walio wengi[6]".**

Na kabla yao Imam Bukhari ameweka mlango katika sahihi yake unaosema:

**«بَابُ ذَبِيحَةِ الْأَمَةِ وَالْمَرْأَةِ»**

**"Mlango wa kichinjwa cha Mjakazi na Mwanamke"**

Amesema Ibn Hajar Allaah amrehemu:

**«كَأَنَّهُ يُشِيرُ إِلَى الرَّدِّ عَلَى مَنْ مَنَعَ ذَلِكَ»**

**"Kana kwamba yeye (imam Bukhari) anaashiria kukosoa juu ya yule aliyekataza hilo[7]".**

---

[5]- Al-Majmuu' (Jz. 8, Uk. 405).
[6]- Nailul autwaar (Jz. 8, Uk. 160).
[7]- Fat-hul baari (Jz. 9, Uk. 932).

Na vivyo hivyo Ahlul kitaab pia ni halali kula vichinjwa vyao hata kama wazazi wa huyo aliyechinja si katika Ahlul kibaab.

Ama asiyekuwa katika Ahlul kitaab si halali kichinjwa chake kwa ujumla wa kauli yake Allaah:

﴿وَطَعَامُ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ حِلٌّ لَّكُمْ وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَّهُمْ﴾

**"Na chakula cha waliopewa kitabu ni halali kwenu[8]".**

Amesema Al-khaazini Allaah amrehemu katika tafsiri yake:

«وَأَجْمَعُواْ عَلَى تَحْرِيْمِ ذَبَائِحِ الْمَجُوْسِ وَسَائِرِ أَهْلِ الشِّرْكِ مِنْ مُشْرِكِي الْعَرَبِ وَعَبَدَةِ الْأَصْنَامِ وَمَنْ لَا كِتَابَ لَهُ»

**"Wamekubaliana juu ya uharamu wa vichinjwa vya majusi (waabudia moto) na baki ya washrikina ambao ni washirikina wa kiarabu, waabudia masanamu na yule asiye na kitabu (si Myahudi wala Mnaswara)[9]".**

3. Awe amekusudia kuchinja, lau kama alimchinja mnyama kwa bila kukusudia ima kwa kujihami ili mnyama asimuumize, au alikusudia kukata kitu kingine lakini tahamaki akamchinja mnyama, basi si halali mnyama huyo kuliwa, kwa kauli ya Allaah:

﴿إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ﴾

**"ila mkidiriki kumchinja"**

[8]- Surat Al-Maida/5.

[9]- Tafsiirul Khaazin (Jz. 2, Uk. 13).

Allaah ameegemeza kitendo cha kuchinja kwa anao wazungumzisha, kwa hiyo mwenye kufanya kitendo hicho atahitajia nia kwa sababu kila amali inahitaji nia:

«إِنَّمَا الأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ، وَإِنَّمَا لِكُلِّ امْرِئٍ مَا نَوَى»

**"Hakika amali zote zinahitaji nia, na hakika kila mtu atalipwa vile alivyonuwia[10]".**

4. Asichinje kwa kumkusudia asiyekuwa Allaah[11], kama kujikurubisha kwa sanamu, mzimu, kaburi, au kuchinja kwa kukumsudia Mfalme, Rais au mheshimiwa fulani, akichinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah mnyama huyo si halali kuliwa hata kama atatamka Bismillaahi, kwa hadithi inayosema:

«وَلَعَنَ اللهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللهِ»

**"Allaah amlaani aliyechinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah[12]".**

5. Asitaje lisilo kuwa jina Allaah, kama vile jina la Nabii (Bismi Nnabiy), Malaika: (Bisimi Jibril), au mzimu fulani n.k.

   Allaah amesema:

﴿حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهِلَّ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ﴾

**"Mmeharimishiwa nyamafu (mzoga), damu, nyama ua nguruwe na mnyama aliye chinjwa kwa (kutajwa) lisilo kuwa jina la Allaah[13]".**

---

[10]- Bukhari (1). Muslim (155).

[11]- Kama vile Shetani, Mzimu n.k.

[12]- Muslim (43).

[13]- Suratul Maida/3.

Amesema Ibn Kathiir Allaah amrehemu katika kutafsiri aya hii:

«مَا ذُبِحَ فَذُكِرَ عَلَيْهِ اسْمُ غَيْرِ اللَّهِ، فَهُوَ حَرَامٌ: لِأَنَّ اللَّهَ أَوْجَبَ أَنْ تُذْبَحَ مَخْلُوقَاتُهُ عَلَى اسْمِهِ الْعَظِيمِ، فَمَتَى عُدِلَ بِهَا عَنْ ذَلِكَ وَذُكِرَ عَلَيْهَا اسْمُ غَيْرِهِ مِنْ صَنَمٍ أَوْ طَاغُوتٍ أَوْ وَثَنٍ أَوْ غَيْرِ ذَلِكَ، مِنْ سَائِرِ الْمَخْلُوقَاتِ، فَإِنَّهَا حَرَامٌ بِالْإِجْمَاعِ

**"Mnyama yoyote aliye chinjwa halafu likatajwa juu yake lisilokuwa jina la Allaah huyo ni haramu, kwa sababu Allaah amewajibisha wachinjwe viumbe (wanyama) wake juu ya jina lake tukufu, na wakati wowote akiepushwa (mnyama) huyo na hilo halafu likatajwa juu yake jina la mwingine (asiyekuwa Allaah), ambaye ni sanamu, shetani, mzimu, au kitu kingine katika baki ya viumbe, basi mnyama huyo ni haramu (kuliwa) kwa makubaliano ya maulamaa[14]".**

6. Ataje jina la Allaah juu yake, kwa ajili ya kauli yake Allaah:

﴿فَكُلُوا۟ مِمَّا ذُكِرَ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ إِن كُنتُم بِـَٔايَٰتِهِۦ مُؤْمِنِينَ﴾

**"Basi kuleni katika walio somewa jina la Allaah juu yake. Mkiwa nyinyi mnaziamini Aya zake[15]".**

Na pia amesema:

﴿وَلَا تَأْكُلُوا۟ مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُۥ لَفِسْقٌ﴾

**"Wala msile katika wale wasio somewa jina la Allaah juu yake. Kwani huo ni upotofu[16]".**

Na Mtume swala na salamu zimshukie amesema:

«مَا أَنْهَرَ الدَّمَ، وَذُكِرَ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ فَكُلُوهُ

---

14- Tafsiri ibn kathiir (Jz.3, Uk. 17).
15- Suratul An-aam/118.
16- Suratul An-aam/221.

**“Kitu chochote ambacho kimemwaga damu[17] na likatajwa jina la Allaah juu yake (mnyama huyo), basi kuleni[18]”**

- Na sharti ni kwamba atamke jina la Allaah wakati wa kupatikana kitendo hicho cha kuchinja wala pasiwepo na kipambanuzi chochote, (mfano) akasema (Bismillaahi) kisha akaenda kunywa maji halafu akarejea na kumchinja mnyama huyo, kwa sababu hiyo ni dhikri maalumu ambayo sharti lake ni kuwa itamkwe wakati wa tukio, na kama ni kipambanuzi kidogo kiasi cha kumlaza mnyama vizuri na kumchinja hapana tatizo.
- Atamke jina la Allaah kwa mnyama aliyemkusudia kumchinja, akitamka hali ya kuwa amemshika mbuzi kisha akabadilisha na kumchukua mwingine basi atamke upya.
- Inatakiwa atamke jina la Allaah: Bismillaahi.
- Haifai mtu kuacha kutamka jina la Allaah (Bismillaahi) makusudi, kwa sababu Mtume swala na salamu zimshukie ameweka sharti kwa mnyama ili awe ni halali kuliwa basi kitumike kitu chenye kumwaga damu na litajwe juu yake jina la Allaah, mpaka baadhi ya maulamaa wanaona kwamba kutamka Bismillaahi wakati wa kuchinja ni sharti na lau mtu aliacha kwa ujinga au kusahau basi mnyama huyo si halali kuliwa (ni mzoga), na baadhi yake wanaona kuwa ni sunna kwa hiyo mtu akiacha kutamka bado mnyama atakuwa ni

---

[17]- Anakusudia kitu chochote kinachoweza kuchinja na kikamwaga damu, sawa ni Kisu, kigae (chupa) au jiwe lenye makali n.k ni halali kukitumia katika kuchinja.
[18]- Bukhari (2488) na Muslim (24).

halali, kwa hiyo muislamu anatakiwa kupatiliza jambo hili wala asiche kutaja jina la Allaah wakati wa kuchinja.

- Asiikusudie Bismillaahi kwa moyo bali aitamke kwa ulimi, na akiwa hawezi kama vile bubu basi itatoa ishara pekee.

7. Achinje kwa kitu chenye makali (chenye kukoa) lakini si kucha wala jino, kwa sababu kucha ni mfupa, na haifai kuchinja kwa kutumia mfupa wa aina yoyote, vile vile kucha, kwa sababu ni kisu wahabeshi, na baadhi ya maulamaa wanasem sababu ya kukatazwa kwake ni:.

    a) Itapelekea watu kufuga kucha kwa ajili ya kuzitumia katika kuchinja, na kama inavyojulikana katika sheria ya kiislamu kwamba haifai mtu kufuga kucha.
    b) Kuchinja kwa kutumia kucha ni kujishabihisha na ndege au wanyama wakali wenye kushambulia ambao sisi tumefadhilishwa juu yao na tumekatazwa kujifananisha nao.

8. Kuhakikisha kwamba anamwaga damu, na hilo lina hali mbili:

    a) Endapo mnyama imeshindikana kumkamata ima kwa kuwa amekimbia au ametumbukia kisimani kiasi ambacho haiwezekani kumpata na kumchinja kwa njia ya kawaida, basi katika hali hii atapigwa kwa kuchomwa sehemu yoyote ya mwili wake mpaka afe, na iliyo bora itumike zana ambayo itaweza kumchoma na kumuua kwa haraka, wala lisitumike mfano wa rungu au fimbo n.k, kwa sababu havimwagi damu.

b) Ama akiwa ni mnyama ambaye anaweza kudirikiwa basi ni sharti achinjwe katika shingo yake, kwa kukata mshipa mkubwa wa pumzi, mshipa wa chakula na kinywaji, na mishipa miwili minene iliyozunguka mshipa wa pumzi na mshipa wa chakula na kinywaji.

9. Awe mchinjaji ameruhusiwa kisheria, na kama hajapewa ruhusa kisheria basi ana hali mbili:

a) Ni kuwa amezuiwa kuchinja kwa ajili ya haki ya Allaah, mfano kuwinda kwa mtu aliyehirimia Hija au Umra, mtu huyo akiwinda mnyama, akamchinja hali ya kuwa amehirimia basi mnyama huyo ni haramu kuliwa, kwa kauli ya Allaah:

﴿وَحُرِّمَ عَلَيۡكُمۡ صَيۡدُ ٱلۡبَرِّ مَا دُمۡتُمۡ حُرُمٗاۗ﴾

**"Na mmeharimishiwa kuwinda wanyama wa bara muda wa kuwa mmehirimia[19]".**

b) Au amezuiwa kwa ajili ya haki ya mwanadamu, mfano kumchinja mnyama ambaye hammiliki wala hajapewa ruhusa na mwenyewe, au mnyama wa wizi n.k. ni haramu kula mnyama huyo kwa mchinjaji na kila aliyejuwa kuwa mnyama huyo si halali.

*****************************************

[19]- Suratul Maida/96.

### Adabu wakati kuchinja:

Kama ilivyokuwa kuchinja kuna masharti ambayo huzingatiwa basi pia kuna adabu ambazo inapasa kuzijua, miongoni mwa hizo:

1. Kumuelekeza mnyama upande wa kibla.
2. Kumtendea wema, kama vile kutumia kifaa chenye makali kupitisha mkono wake kwa nguvu shingoni kwa mnyama.
3. Ngamia huchinjwa hali ya kuwa amesimama kwa kwa miguu mitatu na huku mguu wake wa kushoto ukiwa umenyanyuliwa juu umefungwa, na anachinjwa kwa kutobolewa chini ya kitobwe (chini) ya shingo yake.
4. Asiyekuwa ngamia huchinjwa hali ya kuwa amelazwa kwa ubavu wake wa kushoto na huku mchinjaji akiweka mguu wake juu ya shingo yake, na anayetumia mkono wa kushoto basi atamlaza kwa ubavu wa kulia, na ashike kichwa chake na kukinyanyua kidogo ili one vizuri mahala pa kuchinja, na wala asimzuie mnyama mikono na miguu yake wakati wa kumchinja lakini ikipelekea kufanya hivyo basi iwe kwa upole kiasi cha kuweza kujitikisa ili kutoka damu kwa wingi.
5. Kukamilisha kukata mshipa wa pumzi, mshipa unaopita chakula na kinywaji, mishipa miwili migumu iliyo pembezoni mwa mshipa wa pumzi na mshipa wa chakula na kinywaji.
6. Anatakiwa asitoe kisu chake isipokuwa wakati wa kuchinja.
7. Kuleta takbira baada ya kutaja jina la Allaah: (Bismillaahi wallaahu akbar).
8. Kutaja jina la mmiliki wa mnyama huyo wakati wa kuchinja Ud-hiya au ‘Aqiqa, na kama hakutaja lakini akawa amekusudia hivyo katika moyo wake itafaa.

9. Kuomba dua baada ya kumaliza kuchinja, kama alivyofanya Mtume swala na salamu zimshukie:

«بِاسْمِ اللهِ، اللهُمَّ تَقَبَّلْ مِنْ مُحَمَّدٍ، وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَمِنْ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ»

**"Bismillaahi, ewe Allaah mkubalie Muhammad, Jamaa zake, na umati wake (wote)[20]".**

**************************************

## Mambo ya karaha wakati wa kuchinja

1. Kuchinja kwa kutumia kifaa kisicho na makali.
2. Kumchinja mnyama mmoja hali ya kuwa mwenzie anatazama.
3. Kumfanyia mambo ya karaha kabla ya kumchinja, kama vile kumvunja moja ya kiungo chake, bali kauli sahihi ni uharamu wa jambo hilo.
4. Kunoa kisu hali ya kuwa mnyama anakiona.

Wallaahu A'lam.

**Namuomba Allaah atupe elimu yenye manufaa, atutakabalie ibada zetu na atughufirie madhambi yetu.**

**Markaz sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah**
**Al-khamis9/dhul hijja/1441H – 30/7/2020M**
**Tanga Pongwe.**

[20]- Muslim (19).